

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RAIS DKT. JOHN MAGUFULI ASHUSHA NEEMA DAR ES SALAAM.**

Wananchi wa Mkoa wa Dar es salaam wameendelea kula Matunda ya Serikali ya awamu ya tano baada ya Rais Dr. John Magufuli kutoa zaidi Shilingi Billioni 250 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi Mkakati ya kuziwezesha Halmashauri za Jiji hilo kujiendesha zenyewe ili kupunguza utegemezi wa fedha kutoka Serikali kuu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda amesema miongoni mwa miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kisasa cha Mabasi ya Mikoani Mbezi Luis kitakachogharimu zaidi ya shilingi Billion 50 ambacho ujenzi wake utaanza Mwezi June na kuchukuwa miezi 18 kukamilika.

RC Makonda amesema jengo hilo litakuwa na gorofa tano ambapo kituo hicho cha kisasa kitakuwa na uwezo wa kuchukuwa Mabasi 200 na Maegesho magari 300 (Underground parking) ambapo ndani ya kituo kutakuwa na huduma zote muhimu ikiwemo Hotel, Hostel, Shopping Mall, Maduka, Migahawa, sehemu za mapumziko, Kituo cha Polisi, Bustani, Bank, Vyoo vya kisasa pamoja na Ofisi za kampuni za Magari.

Aidha RC Makonda amesema miradi mingine ni Ujenzi wa Soko la kisasa Kisutu litakalogharimu shilingi Billion 16, Kituo cha Mabasi Chamanzi Mkondogwa, Ujenzi wa Machinjio ya kisasa Vingunguti yenye thamani ya Billion 8.5 itakayokuwa na uwezo wa kuchinja Ng'ombe 1,000 kwa siku hali itakayoondoa uagizwaji wa Nyama Nje ya nchi kwa ajili ya kuuzwa kwenye Hotel na Supermarket ambapo kukamikika kwa mradi huo utawezesha wazawa kupata soko la nyama la uhakika, Ujenzi wa Soko la Mburahati Billion Billion 2.7 kituo

cha Daladala Tuangoma, Soko la Kibada Billion 14 pamoja na miradi mingine mingi ikiwemo Fukwe za Coco, Ujenzi wa Shopping Mall na miradi mingine lukuki inayofanywa na Rais Magufuli kwenye Mkoa wa Dar es salaam.

RC Makonda amemshukuru Rais Magufuli kwa dhamira njema ya kusaidia kutatua kero za wananchi ambapo amewasihi wananchi wa Dar es salaam kukaa mkao wa kula kwa kuchangamkia fursa za ajira zitakazotolewa kwenye miradi hiyo.

HUU NI UPENDO WA DHATI WA RAIS MAGUFULI KWA WANANCHI WAKE.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

10/05/2018